

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

Anuani ya Simu "USTAWI"  
Simu Nambari 2184631.  
Unapojibu tafadhali taja:



IDARA YA USTAWI WA JAMII,  
S. L. P. 1949,  
DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. GA.112/291/02/23

25/06/2008

Mkurugenzi Mtendaji  
Human Development Trust,  
P.O. Box 65147,  
DAR ES SALAAM

**HUMAN DEVELOPMENT TRUST  
RECEIVED**

DATE: 17/7/08

**Kuh: KUSAJILIWA KAMA MTOA HUDUMA KWA MAKUNDI  
YALIYO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZAIDI.**

Kwa niaba ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nachukua fursa hii kukupongeza, kuipongeza taasisi yako NGO kuhusu huduma kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi (Makundi maalum). Taasisi za kidini na kijamii, mashirika, na taasisi yako ikiwa mojawapo mmeonyesha moyo wa kuguswa kuisaidia serikali pale ambapo pana mapungufu kwa kushirikisha jamii kutoa misaada mbalimbali ya kifedha, mitaji midogo, watoto kupatiwa vifaa vya shule, uniform kule jamii walipo wakishirikiana na viongozi wa kata, vijiji na familia.

Aidha kwa mujibu wa sheria, miongozo na kanuni za utoaji huduma hizo kwa makundi maalum. Idara ya Ustawi wa Jamii husajili kwa sheria ya Childrens Home Act pale tu taasisi inapotaka kuanzisha na kuendesha makao ya watoto wenye shida, wa mitaani, wenye ulemavu. Hapo Kamishna anayo mamlaka kisheria kusajili na kusimamia uendeshaji wa makao ya watoto.

Mtizamo wa serikali ni huduma hizi zitolewe kule jamii walipo na Shirika lako Human Development Trust (HDT) limekidhi hitaji hilo.

Wizara inatoa tamko rasmi la kutambua huduma ya taasisi yako ni za Ustawi wa Jamii na Taasisi hii ni mdau mmoja wapo kwa utoaji huduma kwa makundi maalum kwa kuchangia jitihada za serikali na jamii kwa kutoa misaada mbalimbali.

G.A. Kameka

**KAMISHNA WA USTAWI WA JAMII**